BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika,
Napenda kutumia fursa hii adhimu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma, Muumba Mbingu na Ardhi pamoja na vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia neema ya uhai na uzima katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku kwa hali ya amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika,
Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti wa Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii mbele ya Baraza lako Tukufu, Ripoti ambayo inaonesha shughuli zetu zote ambazo tumezitekeleza katika kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Spika,
Kamati ya Ustawi wa Jamii imeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na Kanuni 107(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020).

Mheshimiwa Spika,
Naomba kutumia nafasi hii tena kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa mashirikiano yao makubwa ambayo yameiwezesha Kamati yetu kufanyakazi kwa ufanisi na uweledi mkubwa. Kwa ruhusa yako sasa naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe hao pamoja na Makatibu wa Kamati kama ifuatavyo:-

| Nam. | Jina | Wadhifa |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Shaaban Ali Othman | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Zawadi Amur Nassor | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| 9. | Ndg. Mussa Issa Mussa | Katibu |
| 10. | Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

Mheshimiwa Spika,
Katika utaratibu uliowekwa katika kazi za Kamati kwa muda wote uliopita, Kamati yetu ilipanga kufuatilia utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara zifuatazo:-

1. Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

2. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.
3. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika,
Kwa mwaka huu wa fedha 2021/2022, Kamati ya Ustawi wa Jamii ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita (6) baina ya Unguja, Pemba na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika,
Baada ya maelezo hayo, sasa naomba nianze kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti wa Kamati hii ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama inavyoelekezwa na Kanuni 109(15) ya Kanuni za Kudumu za Baraza (Toleo la 2020).

## WIZARA YA AFYA, USTAWI WA JAMII, WAZEE, JINSIA NA WATOTO

Mheshimiwa Spika,
Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto ni moja miongoni mwa Wizara muhimu katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambapo Wizara hii inagusa moja kwa moja wananchi pamoja na jamii ya Zanzibar. Sambamba na hilo, Wizara hii ina dhamana kubwa ya kuhakikisha kwamba wananchi wote wanafaidika na huduma bora za afya zinazotolewa katika Hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika,
Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikuwa na programu zifuatazo:-

(i) Programu Kuu ya Kinga na Elimu ya Afya;
(ii) Programu Kuu ya Tiba;
(iii) Programu Kuu ya Hifadhi ya Jamii, Maendeleo ya Jinsia na Watoto;
(iv) Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara; na
(v) Programu Kuu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mheshimiwa Spika,
Programu hizo zinatekelezwa kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, ambapo zinaundwa na Idara Saba (7), Taasisi sita (6) na Mabaraza saba (7) ya Taaluma mbali mbali za Kiafya.

## PROGRAMU KUU YA HOSPITAL YA MNAZI MMOJA

Mheshimiwa Spika,
Kamati imebaini uwepo wa changamoto kubwa ya ukosefu wa fedha za OC zinazoingizwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, hali inayopelekea kuzorota kwa utekelezaji wa utoaji wa huduma zinazotolewa katika Hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika,
Hali hii inatokana na uingizaji mdogo wa fedha kinyume na fedha zilizopangwa kwa mujibu wa Bajeti iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi, kwa ajili ya robo mwaka ambapo kwa kila robo ya mwaka Hospitali ya Mnazi Mmoja ilipangiwa kutumia shilingi milioni 400,000,000/=, lakini kwa sasa kwa kila robo ya mwaka wanaingiziwa shilingi

milioni mia moja (100,000,000/=) tu sawa na asilimia 25 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zote za Uendeshaji na Utawala wa Hospitali.
Kwa mnasaba huo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwaingizia fedha zilizopangwa kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa wakati, ili kuweza kutoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wanaofikisha katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika,
Sambamba na hilo, Kamati inaona kushindwa kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kufikia malengo waliyojipangia kunatokana pia na kuwepo kwa changamoto ya madeni makubwa inayodaiwa Hospitali hiyo na Taasisi, Kampuni pamoja na Mashirika mbali mbali yanayotoa huduma za uletaji wa vifaa tiba na dawa. Ambapo hadi tunawasilisha Muhtasari huu wa Ripoti Hospitali ya Mnazi Mmoja inadaiwa Shilingi Milioni 270,000,000/=.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inasikitishwa sana kwa kuona Hospitali wa Mnazi Mmoja inasuasua katika utekelezaji wa majukumu yake kutokana na kadhia ya madeni makubwa yanayowasababishia baadhi ya "Suppliers" kukatisha uletaji wa vifaa tiba pamoja na baadhi ya dawa zinazohitajika kutumika katika Hospitali hiyo. Kutokana na hali hiyo, inaweza kufika wakati Hospitali ya Mnazi Mmoja ikashindwa kutoa huduma zinazohitajika kwa wakati kwa wagonjwa wanaofika kwa ajili ya kupatiwa huduma hizo za matibabu.

Mheshimiwa Spika,
Vile vile, Kamati imebaini kutokuwepo kwa Madaktari Bingwa wa Kugundua Magonjwa ya Akili katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhamasisha wanafunzi waliovyuoni kusomea masomo ya Matibabu hayo, ili kuweza kupata watalamu wetu wazawa waliobobea katika kutoa huduma hiyo.
Pia Serikali kutoa ajira kwa wataalamu waliopo ili kukidhi haja. Kama inavyofahamika maradhi haya hivi sasa yamechukua asilimia kubwa katika jamii zetu na kupelekea kuathiri watoto pamoja na vijana wetu ambao nguvu kazi ya Taifa la sasa na baadae.

## PROGRAMU KUU YA TIBA

Mheshimiwa Spika,
Programu hii ina jukumu la kusimamia utoaji wa huduma katika hospitali za vijiji, hospitali za Wilaya na hospitali za Mkoa. Pia, inahusika na utoaji wa huduma kupitia Mpango wa Damu Salama, Ushauri kwa Hospital Binafsi, Uchunguzi wa Maradhi na kusimamia uendeshaji wa shughuli za Mabaraza ya Kitaaluma pamoja na Huduma za Mkono kwa Mkono. Ambapo, huduma hizo zinatolewa kupitia Programu Ndogo ya Huduma za Matibabu na Huduma za Uchunguzi.

## PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA ZA MATIBABU

Mheshimiwa Spika,
Kamati inasikitishwa na uwepo wa madeni makubwa ya muda mrefu ya watafiti wa nje na wa ndani wanaofanyakazi za tafiti za afya katika Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar pamoja na Wajumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Spika,
Kamati ilipochunguza kwa undani zaidi iligundua kwamba madeni haya yanatokana na kukosekana kwa fedha iliyowahi kuingizwa kwa ajili ya Taasisi hii kama bajeti ya Baraza la Wawakilishi inavyoidhinishwa kila mwaka tangu kuanzishwa kwa Taasisi hii mnamo mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika,
Taasisi haina magari kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku. Vile vile, Kamati haikufurahishwa kwa kuona gari inayotumika kwa ajili ya usafiri wa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo ni chakavu na mbovu sana, ambayo inampelekea kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kila siku kwa weledi, ufanisi na wakati pia haiendani na hadhi ya Taasisi hiyo na wala haiwezi kumudu shughuli zilizopo.

Mheshimiwa Spika,
Hali hiyo, inatokana na kupatiwa gari iliyokuwa ya Wizara ambayo haitumiki tena katika gari zilizokuwa chakavu na kutakiwa kufanya matengenezo, ili aweze kutumia kama usafiri wa Mkuu wa Taasisi katika utekelezaji wa majukumu yake ya kiofisi.

Mheshimiwa Spika,
Kutokana na kadhia hii, Kamati inaishauri Serikali kulitafutia ufumbuzi wa haraka iwezekanavyo tatizo la ukosefu wa usafiri kwa Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Afya – Binguni pamoja na Taasisi yenyewe, ili kuondokana na changamoto ya ufanyaji kazi katika mazingira magumu na yasiyoridhisha.

Mheshimiwa Spika,
Changamoto nyengine wanayokumbana nayo Taasisi hii ni malalamiko ya wananchi yanayotokana na Agizo la Mheshimiwa Rais wetu wa Zanzibar wa Awamu ya Nane Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi juu ya kutokuwepo kwa ajira kwa vijana wa Binguni, vijana ambao walijitolea tokea hatua za awali za ujenzi wa Taasisi hiyo na kushiriki kikamilifu katika kazi mbali mbali.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu wa Baraza la Wawakilishi kukaa na kulitafutia ufumbuzi suala la kupatiwa

ajira kwa vijana wa Binguni walioshiriki katika ujenzi huo kama ahadi iliyotolewa na Kiongozi wetu kwa nyakati mbili tofauti, wakati wa Uwekaji wa Jiwe la Msingi na wakati wa Uzinduzi Rasmi wa Taasisi hiyo.

Mheshimiwa Spika,
Licha ya mafanikio makubwa yanayopatikana kutokana na Usajili wa Madaktari kupitia Baraza la Madaktari Zanzibar bado Baraza hili linakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa bajeti katika kutekeleza majukumu yao walioyojipangia kwa mwaka wa bajeti husika, kutokana na fedha zote wanazozikusanya kupitia Leseni na Vibali vya Madaktari zinaingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina na hatimae hakuna fedha yoyote inayorudi katika Baraza hilo.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inashangazwa na uratibu unaotumika na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa Baraza hili la Serikali kuchukua juhudi kubwa ya ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya ndani na mwisho kulazimika kuziingiza fedha hizo zote kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mheshimiwa Spika,
Kutokuwepo kwa fedha yoyote inayorudi kwa ajili ya kulisaidia Baraza hili. Baraza ambalo halipokei ruzuku wala OC kutoka Serikalini kwa ajili ya kujiendesha katika shughuli zake, hali inayowapelekea kufanya kazi katika mazingira magumu na ya kusuasua, kwani kama inavyofahamika Baraza hili linatakiwa lijitegemee.

Mheshimiwa Spika,
Kutokana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu mzuri wa upatikanaji wa fedha kwa Baraza la Madaktari, kwa ajili ya kuweza kuwasaidia katika uendeshaji wa shughuli zao.

Mheshimiwa Spika,
Kwa upande wa Hospitali zote za Wilaya kwa Unguja na Pemba, Kamati imebaini changamoto mbali mbali zinazopelekea kuzorota kwa utendaji wa kazi zao, kama ifuatavyo:-

Kwanza ukosefu wa upatikanaji wa fedha za OC kwa wakati. Changamoto hii imeonekana na Kamati katika Hospitali zetu zote za Wilaya, ambapo hupelekea kuzorota kwa upatikanaji wa huduma zilizobora na kwa wakati zinazohitajika kutolewa katika Hospitali hizo kwa ajili ya wananchi wanaofika kupatiwa huduma hizo. Mfano halisi ni kama unavyoonekana kwenye Jaduweli hapa chini.

MUHTASARI WA UPATIKANAJI FEDHA KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI KUANZIA OKTOBA - DISEMBA 2021
HOSPITALI YA MICHEWENI

| NO. | Chanzo cha Fedha | Fedha Iliyopangwa Oktoba - Disemba 2021 | Fedha Iliyopatikana Oktoba - Disemba 2021 | Asilimia ya Fedha Iliyopatikana Oktoba - Disemba 2021 |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SMZ | 52,433,500 | 5,712,240 | 10.9 |
| 2. | BUSKET FUND | 7,562,100 | 0 | 0 |
| | **JUMLA** | **59,995,600** | **5,712,240** | **9.5** |

MUHTASARI WA UPATIKANAJI FEDHA KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI KUANZIA OKTOBA - DISEMBA 2021
HOSPITALI YA MAKUNDUCHI

| NO. | Chanzo cha Fedha | Fedha Iliyopangwa Oktoba - Disemba 2021 | Fedha Iliyopatikana Oktoba - Disemba 2021 | Asilimia ya Fedha Iliyopatikana Oktoba - Disemba 2021 |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SMZ | 42,500,000 | 9,720,000 | 22.9 |
| 2. | BUSKET FUND | 3,075,000 | 0 | 0 |
| 3. | HIPZ | 78,000,000 | 72,000,000 | 92.3 |
| | **JUMLA** | **123,575,000** | **81,720,000** | **66.1** |

Mheshimiwa Spika,
Pili ni Ukosefu wa Madaktari Bingwa katika Hospitali zote za Wilaya pamoja na watendaji wengine, hali hii inasababisha kutopatikana kwa huduma ambazo wagonjwa wanahitaji kupatiwa. Kwa mfano, Daktari wa Usingizi pamoja na Daktari wa Mionzi, hivyo masuala ya huduma za upasuaji (*operation*) kufanyika katika mazingira magumu au kutofanyika kabisa kwa baadhi ya Hospitali zetu hizo.

Mheshimiwa Spika,
Kamati, inaishauri Serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini kuwapatia kibali maalum Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa ajili ya kuweza kufanya uajiri wa wataalamu hao wanaokosekana katika hospitali zetu za Wilaya, ili kuondokana na changamoto ambazo zinapelekea kuhatarisha maisha wananchi wetu wanaotumia Hospitiali hizi kwa ajili ya kupata matibabu yaliyosalama na huduma bora.

Mheshimiwa Spika,
Sambamba na hilo, pia kuna upungufu wa dawa na vifaa tiba katika Hospitali zote za Wilaya. Suala hili nalo ni tatizo ambapo katika Hospitali yoyote masuala ya dawa na vifaa tiba ni muhimu, ili kuweza kutoa huduma mbali mbali kwa wagonjwa wanaofika hospitali. Kamati, inaona hali hii inasababisha wananchi au wagonjwa wanapohitaji huduma hata ndogo ya matibabu ya afya basi huacha kuzitumia Hospitali zetu za Wilaya na kukimbilia Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja na kupelekea msongamano na usumbufu mkubwa kwa wagonjwa na wananchi wanafika kwa ajili ya kupata huduma za rufaa.

Mheshimiwa Spika,
Pamoja na Serikali kuchukua juhudi mbali mbali katika Kupiga Vita Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji kwa Wanawake na Watoto. Miongoni mwa juhudi hizo ni Uanzishwaji wa Vituo vya Mkono kwa Mkono, lakini bado vituo hivyo vinakabiliwa na changamoto mbali mbali katika kufikia malengo waliyojipangia.

Mheshimiwa Spika,
Kwanza Dhana ya Kituo cha Mkono kwa Mkono kuwa "One Stop Centre" bado haijafikiwa. Hali hii inasababisha baadhi ya vituo hivyo kukosa baadhi ya watendaji wakiwemo Maafisa wa Ustawi wa Jamii, Daktari au Muuguzi na hata Afisa wa Jeshi la Polisi. Kutokana na hali hiyo, Vituo hivyo kushindwa kufanya kazi masaa ishirini na nne (24), kwa sababu ya ukosefu wa baadhi ya Maafisa na sehemu nyengine kuwepo wachache.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Taasisi tofauti za Serikali zinazoshughulikia Masuala ya Ukatili na Udhalilishaji kwa Wanawake na Watoto kuvifanya Vituo vya Mkono kwa Mkono kuwa "One Stop Centre", yaani kiwe na Maafisa wote wanaohitajika pamoja na kufanya kazi ndani ya masaa ishirini na nne (24), kwani masuala ya kesi za udhalilishaji zinahitaji ushahidi wa haraka.

Mheshimiwa Spika,
Aidha, uchache wa fedha za uendeshaji (OC), kwa ajili ya Vituo vya Mkono kwa Mkono. Kamati, inaona hali hii ya uingizwaji mdogo wa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Vituo hivyo, kwa kweli hakuna kazi itakayoweza kutekelezeka kwa wakati na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika,
Mfano Kituo cha Mkono kwa Mkono Micheweni kwa kipindi cha Oktoba hadi Disemba, 2021 bajeti iliyopangwa ni shilingi Milioni 1,250,000/= na kilichopatikana ni shilingi Lakini 184,000/= tu sawa na asilimia 14.7 kutoka kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika,
Kamati, inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuvipatia fedha Vituo vya Mkono kwa Mkono za kila robo ya mwaka kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa na kwa wakati, ili viweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika,
Pia, kuwepo kwa mashirikiano madogo ya utendaji kazi kati ya Jeshi la Polisi, Maafisa Ustawi wa Jamii, Watendaji wa DPP na Mahkama juu ya ufuatiliaji wa kesi hizo. Kamati, haijafurahishwa na hali hii ya kuwepo kwa mashirikiano madogo miongoni mwa Taasisi hizo za Serikali, ambapo kunapelekea kuzorota kwa uendeshaji wa kesi za Udhalilishaji na hatimae wakati mwengine kufutwa kwa kesi kinyume na utaratibu kwa kisingizio ushahidi haujakamilika.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inazishauri Taasisi zote zinazohusika na Masuala ya Kupinga Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji kwa Wanawake na Watoto zikiwemo Jeshi la Polisi, Maafisa wa Jamii, Madaktari, Watendaji wa DPP pamoja na Mahkama kuzidisha mashirikiano na kufanya kazi kwa karibu zaidi, kuweza kupunguza na hatimae kuvitokomeza kabisa Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji katika jamii yetu na Taifa kwa ujumla, ili iwe historia katika Visiwa vyetu vya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika,
Kwa upande wa Waratibu wa Shehia ambao wanashughulikia Masuala ya Vitendo vya Ukatili na Kesi za Udhalilishaji kwa Wanawake na Watoto nao pia wanakabiliwa na changamoto ya kupatiwa posho ndogo kwa ajili ya kuweza kufuatilia masuala hayo, ambapo kwa mwezi Mratibu mmoja anapatiwa shilingi elfu thelathini (30,000/=), pia upatikanaji wa fedha hizo ni wa kusuasua na kuchelewa kwa muda mrefu takriban inaweza kupita miezi mitatu hadi sita posho isipatikane.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuwaangalia Waratibu wa Shehia kwa jicho la huruma, kwani wao ndio wanaofanya kazi kwa karibu na jamii katika kupambana, kufichua pamoja na kufuatilia masuala hayo ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji kwa Wanawake na Watoto katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika,
Kwa upande wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar, Kamati imebaini uwepo wa uhaba wa fedha za uendeshaji (OC) unaathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi. Hali hii, inapelekea Bohari kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo kununua na kusambaza dawa na vifaa tiba katika Hospitali pamoja na Vituo vya Afya kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuipatia fedha za OC Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar kwa wakati, kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi na kuweza kununua dawa na vifaa tiba na hatimae kusambaza kwenye Hospitali pamoja na Vituo vya Afya vilivyopo Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika,
Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar changamoto nyengine kubwa inayoikabili ni mrundikano wa madeni makubwa na ya muda mrefu yanayotokana na waletaji wa dawa pamoja na vifaa tiba (Suppliers), ambapo hali hiyo imepelekea baadhi ya "Suppliers" kusitisha utoaji wa huduma hizo kwa Bohari kutokana na madeni hayo.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Afya kuandaa kikao cha pamoja baina yao

na waletaji wanaotuletea dawa nchini, ambao wanaidai Bohari Kuu ya Dawa kwa ajili ya utoaji wa huduma za uletaji wa dawa pamoja na vifaa tiba, kwa lengo kufanya mazungumzo ya pamoja katika kutafuta njia muafaka kulipatia ufumbuzi tatizo hili, kwani kubaki kama hali ilivyo sasa kunaweza kuleta athari kubwa ya ukosefu wa dawa na vifaa tiba katika Vituo vyetu vya Afya, Hospitali za Wilaya, Mikoa na hata Rufaa.

Mheshimiwa Spika,
Pia, Kamati inapendekeza kwa Serikali kuzidisha mashirikiano ya Bohari Kuu ya Dawa ya Tanzania Bara (MSD), kwa ajili ya kuagiza Dawa pamoja na Vifaa Tiba, ili Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar iweze kupata dawa pamoja na vifaa tiba kwa wakati na bila ya usumbufu, kwani zote ni Taasisi za Serikali.

## PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA NA UCHUNGUZI

Mheshimiwa Spika,
Kwa upande Wakala wa Dawa, Chakula na Vipodozi (ZFDA), unakabiliwa na uhaba wa wataalamu wa ukaguzi wa mifugo Zanzibar. Hali hii inatokana na kustaafu wataalamu wengi wenye fani hiyo na hivyo inaathiri utendaji wa kazi zao za kila siku za Wakala.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri Serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini kuwapatia ruhusa ya kuweza kuajiri wataalamu wanaohitajika katika nafasi 10 za wataalamu waliostafu, kwa ajili ya kuweza Wakala kufanya kazi zake za kila siku na kuongeza ufanisi katika suala la Ukaguzi wa Mifugo Zanzibar.

Mheshimiwa Spika,
Vile vile, Kamati haikuridhishwa na kuchelewa kukamilika kwa Mradi wa Ujenzi wa Maabara Mpya ya Uchunguzi iliopo Mombasa. Mradi ambao kwa mujibu wa Mkataba ulianza bajeti ya 2018/2019 na ulipangiwa kukamilika mwezi wa Septemba, 2020, lakini mpaka Kamati inawasilisha Ripoti hii Mradi huo bado haujakamilika licha ya kuongezwa kwa muda wa kazi kwa vipindi vinne.

Mheshimiwa Spika,
Aidha, ukosefu wa huduma ya maji na umeme katika Mradi wa Ujenzi wa Jengo Jipya la Maabara ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (ZFDA). Kamati imejionea wakati ilipofanya ziara katika jengo hilo, ambapo hali hiyo itaharibu haiba na ubora wa Maabara hiyo ya Kisasa kwa kukosekana huduma hizo muhimu kwa ajili ya utendaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri Serikali kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) pamoja na Mamlaka ya Maji (ZAWA) kukaa kwa pamoja na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (ZFDA) kwa ajili ya kutafuta njia bora ya kutatua changamoto zilizopo katika jengo jipya la Maabara ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (ZFDA), ili kuweza kuwa na Maabara ya Kisasa yenye Kiwango na Ubora katika utoaji wa huduma zake.

Mheshimiwa Spika,
Kamati pia inaishauri Serikali kuweka utaratibu mzuri wa ulipaji wa malipo ya Mkandarasi pale tu anapokamilisha kazi kwa mujibu wa mkataba, yaani hatua kwa hatua ili kuepusha kutokumalizika kazi kwa wakati na ongezeko la gharama zisizokuwa za lazima kwa visingizio kuwa haya yote yanatokana na ucheleweshaji wa upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika,
Kwa kuendelea na kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti kuhusu Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na mafanikio, lakini bado inakabiliwa na matatizo mbali mbali ya kiutendaji.

Mheshimiwa Spika,
Kutokuwepo kwa malipo kwa baadhi ya Taasisi za Serikali zinazopeleka kazi zao kwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanyiwa vipimo pamoja na uchunguzi. Hali hii inaibebesha mzigo mkubwa Wakala wa Maabara ya Mkemia katika kutekeleza kazi zake za kila siku na kubaki kudai madeni yasiyokuwa na marejesho.

Mheshimiwa Spika,
Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kufuatilia pamoja na kusimamia baadhi ya Taasisi za Serikali ambazo zinapeleka kazi zake kwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanyiwa kazi bila ya kufanya malipo na kuzitaka Taasisi hizo kufanya malipo ya haraka kwa Wakala wa Maabara, ili kuweza kuweza kusaidia kutimiza majukumu yao waliyojipangia.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

Mheshimiwa Spika,
Katika Programu hii Kamati itajikita zaidi katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara kuzungumzia changamoto mbali mbali walizoziona katika suala zima la Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya inayoendelea kutekelezwa kwa upande wa Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika,
Mradi wa Hospitali ya Chake Chake. Kamati imegundua changamoto kadhaa zinazopelekea hadi leo mradi huu kutokamilika kwa mujibu wa muda wa mkataba uliopangwa.

Mheshimiwa Spika,
Haya yote yanatokana na kutokuwepo kwa ushirikishwaji na usimamizi wa karibu kwa

Viongozi wa Juu wa Wizara kwa upande wa Pemba. Jambo hili limebainika pale ambapo Kamati inapohitaji taarifa kuhusiana na miradi husika inayotekelezwa kwa upande wa Pemba huwa taarifa kamili hazipo mpaka Maafisa watoke Unguja.

Mheshimiwa Spika,
Kutokana na kadhia hii, Kamati inapendekeza kwa Serikali kwa miradi yote inayotekelezwa kwa upande wa Pemba kushirikishwa kikamilifu katika hatua zote watendaji wa Pemba, hali hii itasaidia kuondoa changamoto ya sitofahamu kwa baadhi ya viongozi wa Wizara kutokuwa na uelewa wowote kuhusiana na miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika,
Vile vile, Kamati haioni haja kwa miradi inayotekelezwa Pemba kusimamiwa na Maafisa kutoka Unguja wakati ambapo Pemba Maafisa hao wapo lakini hawatumiwi wala hawashirikishwi ipasavyo. Kuendelea na utaratibu huu Kamati inaona ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali, fedha ambazo zingesaidia kutumika katika masuala mengine ya maendeleo kwa ajili ya kuimarisha uchumi wetu, bali zinatumika kwa baadhi ya Maafisa kukodi hoteli, posho za kujikimu pamoja na posho za usafiri.

Mheshimiwa Spika,
Kutokana na hali hiyo, Kamati inapendekeza tena kwa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kusimamia pamoja na kuwashirikisha kikamilifu wataalamu wetu wa ndani katika utekelezaji wa Miradi hii mipya ya IMF inayoendelea ya Ujenzi wa Hospitali za Wilaya ya Mkoa kwa Unguja na Pemba, ili yasijekujirudia yaliyojitokeza katika utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Hospitali ya Chake Chake na Hospitali ya Rufaa ya Binguni, ambapo hadi tunawasilisha ripoti hii tunajiuliza kulikoni? Kwani kuna fedha nyingi ambazo tayari zimeshaidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu wa Hospitali ya Binguni, lakini hadi sasa hatuoni utekelezaji wowote.

Mheshimiwa Spika,
Kwa kuendelea, Kamati inaishauri tena Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kulitafutia ufumbuzi muafaka suala la watendaji watatu (3) wa Kitengo cha Malaria, watendaji ambao wanafanya kazi kwa muda wa miaka 14 bila ya kuajiriwa, ambapo ni kinyume na taratibu za Kiutumishi Serikalini.

Mheshimiwa Spika,
Pia, Kamati inaishauri Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuanzisha pamoja na kuimarisha Vitengo vya Saratani na Mionzi katika Hospitali zetu za Wilaya na Mikoa kwa Unguja na Pemba, ili wagonjwa wanaofika kupata huduma hizi wazipate kwa wakati, kwani Kamati imebaini vitengo hivi vinafanya kazi katika hali ya kinadharia tu.

Mheshimiwa Spika,
Mwisho kabisa kwa Wizara ya Afya, Kamati haikuridhishwa na mazingira ya uendeshwaji wa Kituo cha Kulelea Watoto Yatima cha AL-AHBAB kilichopo Micheweni – Pemba. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara kukifunga Kituo hicho, hii

inatokana na Kamati baada ya kujionea hali halisi iliopo katika kituoni hapo na kufanya uchunguzi wa kina na kubaini kwamba Kituo hiki kina mapungufu mengi ya kisheria katika kuanzishwa kwake pamoja na uendeshaji wake.

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MAFUNZO YA AMALI

Mheshimiwa Spika,
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina Programu Kuu Sita (6) ambazo zinatekelezwa kwa mashirikiano makubwa ya utatu, yaani baina ya Serikali, wananchi, washirika tofauti wa maendeleo wa ndani na nje. Programu hizo ni:-

(i) Programu Kuu ya Elimu ya Maandalizi na Msingi;
(ii) Programu Kuu ya Elimu ya Sekondari;
(iii) Programu Kuu ya Elimu ya Juu;
(iv) Programu Kuu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali;
(v) Programu Kuu ya Ubora wa Elimu; na
(vi) Programu Kuu ya Utawala na Uongozi.

## PROGRAMU KUU YA ELIMU YA JUU

Mheshimiwa Spika,
Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kinakabiliwa na changamoto ya mzigo mkubwa wa madeni yanayoendelea kulipwa kutoka kwa watoa huduma pamoja na wafanyakazi wa ndani. Hali hii hupelekea kutumika kiasi kikubwa cha bajeti kulipia madeni makubwa ya utekelezaji wa kazi zilizopita ambayo Chuo kimekuwa kikilipa tangu Mwaka 2019 ambapo Deni lililokuwa likidaiwa Chuo ni Bilioni 2.5 na hadi kufikia 2021/2022 deni limefika zaidi ya Bilioni 3, ambapo madeni haya yanatokana na walimu wa muda (part timers), Ujenzi wa Dakhalia za Wanafunzi pamoja na Ujenzi wa Nyumba za Walimu, Ununuzi wa Kompyuta, madeni ya watendaji ya 'Over time', likizo pamoja na fedha za ufiwa.

Mheshimiwa Spika,
Ambapo Deni la ZSSF tu kwa ujenzi wa dakhalia za wanafunzi Chuo cha Chwaka pamoja na deni la ujenzi wa nyumba za walimu mpaka kufikia June, 2020 limebakia 838,657,640,41/=, yote haya yanapelekea mzigo mkubwa kwa Chuo na hatimae kuzorotesha shughuli za utendaji wa Chuo.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Uongozi wa Chuo Kikuu cha SUZA kukaa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kulitafuta njia sahihi ya kuwasaidia Chuo kuweza kuyalipa madeni yanayokabiliana nayo hali inayowapelekea hata asilimia ya utekelezaji kushuka siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika,
Uhitaji mkubwa wa ukarabati wa miundombinu kutokana na uchakavu wa majengo, ambapo Kamati hii wakati walipokuwa wakipokea taarifa ya utekelezaji wa robo ya pili ya mwaka wa fedha 2021/2022 waligundua kwamba Ukumbi wa Dr. Shein tu kila

mwaka unatumia Milioni 50,000,000/= kwa ajili ya ukaratibu wa jengo kila ifikapo wakati wa mahafali ya Chuo. Hii inatokana na changamoto ya paa lote kuvuja, madirisha pia kupitisha maji na Kamati ilipokwenda ndani zaidi ikabaini kuwa ujenzi huu kikweli haukukidhi viwango. Sambamba na hilo, Kamati pia imebaini Eneo Jipya lilojenga la IT ndani ya Chuo hiki pia linavuja.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaendelea kuishauri Serikali na Wizara husika pale inapotokezea Miradi ya Ujenzi ni vyema kuwashirikisha wataalamu wetu wa ndani pamoja na Wakala wa Majengo ya Serikali (ZBA), ili kuondokana na kasoro za baadae kama ilivyo sasa kwa Ukumbi wa Dr. Shein uliopo Tunguu na Eneo la Kompyuta liliopo ndani ya Chuo ambapo linavuja kabla hata hawajafanya makabidhiano ya mwisho.

Mheshimiwa Spika,
Sambamba na hilo, Chuo kufuata Muundo wa Utumishi wa Umma hii ni miongoni mwa changamoto kubwa inayopelekea walimu wengi kuondoka kutokana na maslahi madogo wanayolipwa ukilinganisha na Vyuo vyengine nchini hali inayopelekea Vyuo vyetu kukosa wataalam wabobezi katika fani zinazotolewa ndani ya Chuo hicho.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri Serikali kufanyika kwa kikao cha pamoja baina na Wizara ya Elimu na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora juu ya kulitafutia ufumbuzi suala zima linalohusiana na Muundo wa Vyuo Vikuu vya Zanzibar, kwani kuendelea kufuata Muundo wa Utumishi wa Umma ni kwenda kinyume na Taratibu na Kanuni za Vyuo Vikuu Duniani.

Mheshimiwa Spika,
Chuo cha Utalii Maruhubi, Kamati imebaini kuwepo kwa upotevu wa Rasilimali za Serikali kutokana na kununuliwa kwa mashine kwa ajili ya kutoa huduma bora za Kituo cha Kufulia (Laundry), lakini matokeo yake mashine hizo mpya, kubwa na wala hazijawahi kutumika zimewekwa katika mazingira sio rafiki, ambapo Kamati inawasiwasi kuharibika kwa mashine hizo na huo itakuwa ni ubadhirifu na uhujumu uchumi wa mali za Serikali.

Mheshimiwa Spika,
Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia SUZA kukifanyia matengenezo Kituo cha Kufulia (Laundry), ili mashine ziwekwe kwenye mazingira rafiki na kiweze kutumika na Taasisi za Serikali pamoja na watu binafsi, kwani mashine zao ni kubwa tena za kisasa na kuweza kuongeza pato kwa Chuo na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Spika,
Kwa upande wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KIST) Wanafunzi wa Shahada ya Kwanza kukabiliwa na madeni ya ada, kutokana na kupatiwa asilimia ndogo

ya mkopo wanaoupata kutoka katika Bodi ya Mkopo ya Elimu ya Juu Tanzania. Hii inawakabili haswa wanafunzi wetu wanaojiunga na "Course za Air Craft" kutokana na kutolipiwa kama Course nyengine hali inayowapelekea wanafunzi waliokuwa washaanza kushindwa kuendelea na masomo yao au kubadilisha Course.

Mheshimiwa Spika,
Course hii gharama yake kwa mwaka mmoja ni shilingi milioni 8,000,000/=, ambapo wanafunzi waliojiunga na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania wanalipiwa shilingi milioni 3,000,000/= tu kwa mwaka, hali inayowasababishia wanafunzi hao kushindwa kukamilisha kiwango cha fedha kilichobakia kwa ajili ya malipo ya ada, ambapo Kamati imegundua kuna baadhi ya wanafunzi kushindwa kuendelea na masomo hayo kutokana na hali ngumu za kimaisha na kurudi nyumbani na wengine kubadilisha Kada za masomo na kusomea masomo mengine nje ya fani zao.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufanya kikao na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania, ili kulipatia ufumbuzi suala la utoaji wa ada ndogo kwa Kada ya "Air Craft", kwani suala hili tayari Kamati ilichukua juhudi ya kulifuatilia pamoja kuliwasisha kwao kwa ajili ya hatua za utatuzi, lakini hadi sasa hakuna mabadiliko yoyote yaliyofanyika baada ya mazungumzo hayo.

## PROGRAMU KUU YA UBORA WA ELIMU

Mheshimiwa Spika,
Licha ya mafanikio mbali mbali yaliyopatikana katika Baraza la Mitihani Zanzibar, lakini bado utendaji wao unakabiliwa na tatizo la kutomiliki majengo kwa ajili ya Vituo vya Usahihishaji wa Mitihani, hali hii huleta usumbufu mkubwa katika zoezi zima la usahihishaji wa mitihani Zanzibar.

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuiomba Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuwapatia maeneo Baraza la Mitihani, kwa ajili ya kujenga majengo maalum ya kusahihishia mitihani, ili kuisaidia Serikali kuondokana na gharama kubwa na zisizo za lazima kwa kukodi majengo ya watu binafsi kwa ajili ya kusahihisha mitihani ambayo sio salama na hatarishi kwa kufanyia kazi hizo za Taifa.

Mheshimiwa Spika,
Vile vile, Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu ina changamoto ya ukosefu wa majengo ya Ofisi. Sheria ya kuanzishwa kwa Ofisi imeanzisha ndani yake Ofisi za Ukaguzi za Mikoa.

Ofisi hizi kwa sasa zipo kinadharia tu. Wakaguzi wamegawika kimikoa na wanatekeleza majukumu yao kwa mgawanyiko wa Mikoa. Hata hivyo, kiutendaji Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kusini Unguja wapo katika jengo la Ofisi Kuu ambalo halina nafasi. Kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Unguja wapo katika chumba kimoja katika majengo ya Ofisi za SUZA – Beit – El – Ras ndicho ambacho kinatumika. Aidha, kwa upande wa Pemba hali ipo kama ilivyo Unguja wapo katika jengo la Maktaba Chake

Chake na kwa Wete wapo jengo la Ofisi ya Elimu Mkoa.

Mheshimiwa Spika,
Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuwapatia maeneo Wizara ya Elimu kwa ajili ya kujenga Ofisi za Wakaguzi wa Elimu Zanzibar katika kila Mkoa, ili kutimiza matakwa ya kisheria ya uwepo wa ofisi hizo kila Mkoa kwa upande wa Unguja na Pemba, ili waondokane na kadhi ya kujibanabana katika Ofisi za Taasisi nyengine kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika,
Jengine ni madeni makubwa wanayodai wakaguzi wetu wa elimu kwa muda mrefu sana na miaka mingi kupita wakaguzi wa elimu hawajalipwa stahiki zao pamoja na posho za kufanyakazi kwenda katika Skuli za Vijijini na Visiwani, hali inayowapelekea kufanya kazi katika mazingira magumu yanayowasababishia wakati mwengine mtu kushindwa kufika katika skuli alizopangiwa kuzifanyia ukaguzi huo, ambapo Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto ya madeni ya wakaguzi wa Elimu wa ndani yanayotokana na kazi ya ukaguzi unaofanywa katika Skuli za Maandalizi, Msingi na Sekondari kama msemo wa Kiswahili unavyosema *"Mtu hulipwa kabla jasho kukauka"*.

Mheshimiwa Spika,
Ongezeko la vitendo vya Udhalilishaji kwa wanafunzi wenye ulemavu bado ni tatizo kubwa kutokana na baadhi ya walimu na jamii kwa ujumla kuendelea kuwadhalilisha wanafunzi hao kutokana na hali zao. Kamati, inasikitishwa na muamko mdogo wa jamii wakiwemo walimu pamoja na wazazi kutokuwa na ujasiri wa kueleza au kufichua vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto kutokana na sababu ikiwemo muhali, kumalizwa kwa masuala hayo chini kwa chini kwani mara nyingi masuala hayo hufanywa na watu wa karibu kama vile wazazi wenyewe au jamaa wa karibu ama majirani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika,
Ambapo hali hiyo, hupelekea kuendelea kwa vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto. Hivyo ni vyema kuachana na masuala ya muhali, kumaliza masuala hayo kinyume na utaratibu, wahusika kutoa taaluma kwa wananchi na jamii kwa ujumla kuhusu kupinga vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto hususan katika skuli zetu ikiwemo Skuli za Elimu Mjumuisho. Kushamiri kwa vitendo hivyo kunatokana na mrundikano mkubwa wa wanafunzi katika madarasa ya Elimu Mjumuisho kunakopelekea walimu kushindwa kutoa uangalizi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika,
Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wakapunguziwa vipindi vya masomo ya kawaida Walimu wa Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, ili kupata muda wa kutosha kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi hao masomo ya Mjumuisho pamoja na Stadi za Maisha,

## PROGRAMU KUU YA UONGOZI NA UTAWALA

Mheshimiwa Spika,
Kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya ucheleweshaji wa utekelezaji wa baadhi ya Miradi ya Ujenzi inayotekelezwa kupitia fedha "IMF" ambapo kwa upande wa wenzetu wa Tanzania Bara takribani miradi kama hii imeshakamilika, imeshakabidhiwa na kuanza kutumika. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuandaa timu maalum ya usimamiaji na ufuatiliaji wa utekelezaji wa hatua mbali mbali za Miradi hiyo, ili kuweza kukamilisha ujenzi wa Skuli hizo zinazojengwa katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba kwa wakati kama masharti ya fedha hizo yanavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika,
Kamati katika kufanya kazi zake za kawaida za ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara imebaini bado kuna tatizo la kukosekana kwa Mitaala ya Watu Wenye Ulemavu wa Akili na Uoni katika Skuli zetu za Elimu Mjumuisho. Kwa mnasaba huo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuandaa Mitaa Maalum ya Watu Wenye Ulamavu wa Akili na Uoni, ili na wao waweze kusoma katika mazingira mazuri, bora na salama katika kujipatia elimu, kwani kama tunavyofahamu haki ya kupata elimu ni ya kila mtu.

Mheshimiwa Spika,
Hili linakwenda sambamba na kutokuwepo kwa miundombinu Rafiki na yenye kufika katika baadhi ya majengo yetu ya Skuli za Maandalizi, Msingi hadi Sekondari hali inayowasababishia Watu Wenye Ulemavu kusoma katika mazingira magumu. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha katika Miradi yote ya Ujenzi inayoendelea kujengwa ya Skuli zote kwa Unguja na Pemba kuwa inazingatia Muongozo uliotolewa na Serikali kuhusu Uwepo wa Miundombinu Rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu, ili waweze kupata huduma kama watu wengi.

Mheshimiwa Spika,
Vile vile, changamoto nyengine ni uwepo wa uhaba wa vikalio pamoja na vitabu vya kusomea katika baadhi ya Skuli zetu. Mfano halisi ni Skuli ya Kwerekwe "H", Kwerekwe "F" pamoja na Skuli ya Kisiwandui kwa wanafunzi wenye ulemavu. Kwa msingi huo, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika suala la kuandaa na kuchapisha vitabu pamoja na vifaa vya kujifunzia na kufundishia kuwazingatia watu wenye ulemavu wakiwemo watu wenye ulemavu uoni hafifu, kwa kuwapatia vifaa ikiwemo vitabu vya nukta nundu, mashine za kuchapia pamoja na vyengine, ili kuweza kupata elimu ambayo ni haki yao kama binaadamu au raia wengine wa Tanzania.

## WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

Mheshimiwa Spika,
Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inatekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu Nne (4) ambazo ni:

(i) Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapishaji;
(ii) Programu ya Maendeleo ya Vijana;
(iii) Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; na
(iv) Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPISHAJI

Mheshimiwa Spika,
Kamati katika kuendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu yake imegundua uhaba wa rasilimali watu na vifaa katika Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) katika Ofisi zake zote za Unguja, Pemba na hata Dar-es-Salaam, ambapo hali hiyo hupelekea kwa baadhi ya wakati kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika,
Aidha, changamoto nyengine ambayo inalikabili Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) ni bajeti ndogo ya kwa ajili ya kuweza kutekeleza majukumu ya *ZBC* – TV na Redio ikiwemo kuandaa vipindi vya nje ya studio, hali inayowapelekea vipindi kurudiwa zaidi ya miezi sita (6).

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuongeza bajeti kwa Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC*) kwa lengo la kuweza kutekeleza majukumu yao ya kila siku ili kuweza kufikia malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika,
Pia, suala la kuwepo kwa mashirikiano madogo baina ya watendaji wa Shirika la ZBC na Idara ya Mawasiliano Ikulu. Hali hii inapelekea Shirika kuchelewa kupata taarifa mapema kuhusu matukio ya Viongozi na badala yake vituo vya Binafsi kupata taarifa hizo mapema.

Mheshimiwa Spika,
Kamati, inaipendekeza kwa Idara ya Mawasiliano Ikulu kufanya kazi kwa mashirikiano ya karibu na Uongozi wa Shirika la Utangazaji (*ZBC*), kwani wao ndio chombo na mdomo wa kuyatangaza masuala yanayotekelezwa na Serikali. Ambapo Kamati imebaini kuna shughuli nyingi za Viongozi wa Kitaifa zinafanyika ndani na nje ya nchi na Shirika kuchelewa kupata taarifa mapema, hali inayowapelekea kuchelewa kufika katika maeneo ya matukio kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika,
Sambamba na hilo, Kamati imebaini uwepo wa malipo madogo katika uendeshaji wa Channel ya ZBC 2, ambapo kwa mujibu wa Mkataba uliopo gharama za uendeshaji kwa kila mwezi Shirika la ZBC linapokea Tsh. Milioni Tano (5,000,000/=) tu kutoka Kampuni ya Azam Media Group.

Mheshimiwa Spika,
Kutokana na malipo hayo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuangalia upya Mkataba huo kwani malipo yanayopatikana kwa ajili ya uendeshaji wa Channel hiyo hayaendani na hali halisi ya uanzishwaji pamoja na uendeshaji wake.

Mheshimiwa Spika,
Katika Shirika la Magazeti la Serikali (SMS) licha ya mafanikio yaliyopatikana, lakini bado linakabiliwa na changamoto ya mauzo madogo ya magazeti ambapo fedha za matangazo ndizo zinafidia gharama za uchapishaji ambazo nazo pia hazikidhi mahitaji ya Shirika katika uendeshaji shughuli zake za kila siku.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri Serikali kulipatia Shirika la Magazeti ya Serikali rasilimali watu pamoja na vifaa ikiwemo Posho Maalum, usafiri pamoja na fedha za OC, kwa ajili ya kuweza kutekeleza kazi zake kwa ufanisi zaidi na kwenda na mabadiliko ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika,
Vile vile, ukosefu wa matangazo katika magazeti ya Zanzibar Mail, Zanzibar Leo Wanawake na Zaspoti, hivyo matangazo yanayopatikana kupitia Zanzibar Leo ndio wanayosaidia uchapishaji wa magazeti hayo.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri Serikali kuzielekeza Taasisi zake zote kutoa matangazo yao na kuchapisha kupitia vyombo vya Umma vya Serikali, kwa lengo la kuvitumia vyombo hivyo pamoja na kuweza kupata mapato, ili kuweza kujiendesha kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inamshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi pamoja na Wizara kwa ujumla kwa Uzinduzi wa "Layout Page" Mpya ya Gazeti la Zanzibar Leo, ambapo Kamati imefurahishwa kwa uzinduzi huo, kwani ulikuwa ni ushauri na mapendekezo ya Kamati hii, hivyo kufanyiwa kazi kwake kulifanya Gazeti kubwa bora na lenye muonekano mzuri zaidi ukilinganisha na magazeti yote Tanzania.

Mheshimiwa Spika,
Licha ya Mafanikio hayo, Kamati inaendelea kuishauri tena Serikali kulitafakari kwa makini suala la upandishaji wa bei ya Gazeti la Zanzibar Leo kutoka Tsh. 500/= kwa sasa hadi Tsh. 100/= haiendani na wakati katika soko. Kamati inaona ni vyema umefika wakati Serikali kulitafakari upya suala, ili Shirika liweze kumudu kupata gharama za uchapishaji pamoja na kuweza kuchangia pato katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mheshimiwa Spika,
Kutokuwepo kwa udhibiti wa bei za watoa huduma hasa kati ya Taasisi za Serikali na ZMUX. ZMUX ilifanya mazungumzo na ZICTIA juu ya kupunguza gharama za huduma ya matumizi ya Mkonga ambapo kwa mwezi wanawatoza shilingi milioni 50,000,000/= hali inayopelekea Kampuni hii kufanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishari Serikali kuandaa kikao cha mazungumzo ya pamoja kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi juu ya suala zima la upandishaji wa bei kati ya Taasisi za Serikali kinyume na utaratibu. Kamati kutokana na kadhia hii haikufurahishwa kuona Taasisi za Serikali zinavutana katika utendaji, wakati wote wapo kwa ajili ya kutoa huduma na kuongeza pato la nchi.

Mheshimiwa Spika,
Pia, Kamati imebaini kuwa Kampuni ya ZMUX inafanya kazi kinyume na taratibu za Sheria kwani hadi Kamati inapokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Oktoba – Disemba, 2021 Kampuni hii haikuwa na Bodi ya Wakurugenzi.

Mheshimiwa Spika,
Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha uteuzi wa Bodi ya Kampuni hii, kubakia kama ilivyo ni kuirudisha nyuma kiendeshaji na kimaamuzi, kwani kama inavyofahamika katika Taasisi kama hizi haziwezi kufanyakazi bila ya uwepo wa Bodi na Uongozi.

Mheshimiwa Spika,
Tatizo jengine baadhi ya Taasisi za Serikali kutopeleka kazi zake kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar pamoja na kuchelewa kulipwa kwa wakati, hali hiyo kupelekea Wakala kushindwa kutekeleza kazi zao kwa ufanisi zaidi na katika hali ya kusuasua.

Mheshimiwa Spika,
Kamati, inaipendekeza kwa Serikali kuhakikisha kwamba Taasisi zote za Serikali zinapeleka kazi zake kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar kama Agizo la Serikali linavyoelekeza pamoja na kulipa kwa wakati, kwa ajili ya Wakala kuweza kujitegemea na kujiendesha wenyewe na kuweza kufikia malengo iliyojipangia. Kamati imebaini sababu kubwa inayoikumba Wakala katika utekelezaji wa shughuli zake ni mrundikano wa madeni makubwa na yasiolipwa kwa muda mrefu, ambapo hadi Kamati inawasilisha ripoti hii inadai Taasisi za Serikali pamoja na Binafsi jumla ya Tsh. Milioni Mia Nne Hamsini na Moja, Laki Nane na Kumi na Tano, Mia Tano na Kumi (451,815,510/=).

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIJANA

Mheshimiwa Spika,
Katika Programu hii Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa baadhi ya miradi iliyotekelezwa na Baraza la Vijana kupitia Vikundi mbali mbali vinavyohusiana na Vijana vilivyoanzishwa katika Shehia za Unguja na Pemba. Ambapo Kamati katika vikundi hivyo ilibaini changamoto kadhaa ikiwemo kutokufanyika kwa Upembuzi Yakinifu kwa miradi ya maendeleo yote iliyoanzishwa kwa Vijana, kutoshirikishwa Vijana kikamilifu katika uibuaji wa miradi, kutopatiwa taaluma kuhusu miradi hiyo inayokusudiwa kutekelezwa katika maeneo yao husika pamoja na ukosefu wa mitaji na masoko kwa bidhaa zinazozalishwa kupitia Vikundi hivyo.

Mheshimiwa Spika,
Kutokana na hali hii imepelekea takribani utekelezaji wa miradi mingi kufeli na kutofikia malengo yaliyokusudiwa katika kuanzishwa kwake ya kuwainua Vijana kiuchumi na kijamii, ili kwenda sambamba na Kauli Mbinu ya Mheshimiwa Rais wetu Mpendwa wa Zanzibar kwamba Vijana kuweza kujiajiri bila ya kusubiria ajira kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika,
Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kuandaa timu ya wataalamu katika uanzishaji na usimamizi wa Miradi ya Maendeleo ya Vijana, kwani Kamati imebaini miradi mingi iliyoanzishwa kupitia Baraza la Vijana haikufanikiwa kutokana na kukosekana kwa utaalamu na usimamizi ulioimara katika Vikundu vinavyopelekewa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika,
Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kupitia Baraza la Vijana kabla ya kuanzishwa kwa miradi ya Maendeleo inayowahusu Vijana ufanyike utafiti wa kina kabla ya kuibua Miradi ya Maendeleo ya Vijana pamoja na kuwashirikisha Vijana kikamilifu katika hatua zote za uanzishaji wa miradi hiyo ndani ya maeneo yao husika, ili kuondokana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Miradi hiyo. Mfano halisi wa Miradi ambayo haikufanikiwa ni Mradi wa "Green House" pamoja na Mradi wa Kilimo cha Pilipili.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Mheshimiwa Spika,
Kamati pia imebaini kuwepo kwa uzorotaji mkubwa wa ukusanyaji wa mapato kwa Baraza la Kiswahili unaotokana na kuwepo kwa mfumo wa zamani wa uuzaji wa vitabu, hali inayopelekea Baraza kushindwa kuuza vitabu hivyo kwa wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika,
Kamati pia, imesikitishwa kuwa tokea kuanzishwa kwake Baraza la Kiswahili hakuna Mzanzibari yeyote aliyewahi kunufaika na fursa za ajira kwa kukitangaza Kiswahili ama kufundisha ndani na nje ya nchi.

Kamati inaishauri Wizara kupitia Baraza la Kiswahili la Zanzibar kuwa wabunifu katika kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi kwa ajili ya uuzaji wa vitabu vyao, ili tuweze kuingia katika Soko la Ushindani kwa upande mmoja na kwa upande wa pili itasaidia kuongeza pato la ndani. Mfano mzuri na wa kuigwa ni Shirika la Mkuki na Nyota lilifika katika Ofisi za Baraza la Wawakilishi Chukwani mwezi wa Mei mwaka 2021 kwa kuuza vitabu tofauti kama vile vitabu vya Mhe. Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mhe. Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mzee Ali Hassan Mwinyi na Mhe. Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Spika,
Hivyo, Kamati inalishauri tena Baraza la Kiswahili la Zanzibar kuandaa Mpango Mkakati wa kuzifikia Taasisi zote za Serikali na Watu Binafsi kwa ajili ya kuvitangaza na kuviuza vitabu, makamusi pamoja na machapisho mengine kwani Wahenga wanasema *"Biashara itangazwayo ndio itokayo"*.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA MIPANGO YA WIZARA

Mheshimiwa Spika,
Katika Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo Kamati imegundua changamoto mbali mbali ikiwemo:-

*(a)* Kutokuwepo kwa usimamizi madhuti katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayohusu Vijana hii imebainika na Kamati wakati wa ziara za kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Mfano wa Miradi hiyo, Mradi wa Ujenzi wa "Green House" 19 kwa Unguja na Pemba, Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vilivyojengwa katika Wilaya 5 kwa Unguja na Pemba ambapo Unguja 3 na Pemba 2 na Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Studio ya ZBC Pemba pamoja na Mradi wa Kilimo cha Pilipili.
*(b)* Kutokuwepo kwa mashirikiano mazuri ya kiutendeaji baina ya Viongozi wa Juu wa Wizara na Watendaji wa chini. Suala hili lilionekana na Kamati wakati wa taarifa za utekelezaji wa Bajeti kwa upande wa Pemba.
*(c)* Uwepo wa uelewa mdogo wa matumizi ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma kwa baadhi ya Wakuu wa Idara kwa upande wa Pemba.
*(d)* Uhaba wa rasilimali watu hususan wataalam wabobezi katika fani tofauti wanaohitajika katika uendeshaji wa shughuli za kila siku za Wizara hii.
*(e)* Kutokuwepo kwa Muundo wa Utumishi katika Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC).
*(f)* Baadhi ya Taasisi za Serikali kutotekeleza Agizo la Serikali la kupeleka kazi zao za Ofisi kwa Wakala wa Uchapaji wa Serikali (ZAGPA).
*(g)* Kuwepo kwa bei ndogo ya Gazeti la Zanzibar Leo kwa muda mrefu.
*(h)* Kutokuwepo kwa stahiki kwa baadhi ya Wakuu wa Vitengo na watendaji wa chini ambazo wanastahiki kupatiwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma ikiwemo "Over times" Posho la Mazingira Magumu

pamoja na Posho la Kushika Nafasi za Uongozi,

Mheshimiwa Spika,
Kamati, inaishauri Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kufanya utafiti mwanzo kabla ya kuibua miradi ya vijana pamoja na kuwashirikisha vijana wenyewe wa maeneo husika, kwa lengo la kuwa na miradi mizuri na itakayoweza kuleta tija kwa Vijana na Taifa kwa ujumla pamoja na kuweza kunusuru upotevu wa fedha nyingi za Serikali.

Mheshimiwa Spika,
Aidha, Kamati inaushauri Uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kutatua tatizo la rasilimali watu pamoja vifaa kwa Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*), ili kuwaweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na weledi.

Mheshimiwa Spika,
Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Taasisi zote za Serikali zinapeleka kazi zake kwa Wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar (ZAGPA) pamoja na kulipa kwa wakati kwa ajili ya Wakala kuweza kujiendesha na kujitegemea wenyewe na kufikia malengo iliyojipangia.

Mheshimiwa Spika,
Pia, Kamati inaishauri Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuzidisha mashirikiano na Taasisi ya *Tanzania Horticultural Association (TAHA)*, kwa ajili ya kupatiwa elimu pamoja na utaalamu kuhusu masuala ya kilimo na mbegu bora kwa Mabaraza ya Vijana kwa lengo la kulima kwa kutumia utaalamu na maarifa mapya, ili kuweza kupata mafanikio makubwa zaidi ya kulima eneo dogo, muda mdogo lakini mafanikio yenye tija kubwa.

Mheshimiwa Spika,
Sambamba na hilo, Kamati inaishauri tena Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuandaa mpango madhubiti wa usimamizi na ufuatiliaji wa Ujenzi wa Miradi ya Maendeleo inayohusu Wizara, ili kuondoa changamoto ya uchelewaji wa ukamilishaji wa miradi hiyo na upotevu wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri tena Serikali kuliangalia upya suala la upandishaji wa bei wa Gazeti la Zanzibar Leo, ambapo bei iliopo ni ndogo na ya muda mrefu na imeshapitwa na wakati ukilinganisha na magazeti mengine nchini Tanzania.

Kamati inapendekeza tena kwa Serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini kukaa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kulishughulikia kwa haraka iwezekanavyo suala la kutokuwepo kwa Muundo wa Utumishi katika Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), hali inayowapelekea watendaji kukosa baadhi ya stahiki zao zilizopo kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika,
Kamati inaishauri Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Idara ya Utumishi ya Wizara kuandaa mpango wa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watendaji wote wa Wizara hii, ili kuendana na mabadiliko yanayojitokeza kwa Tasnia ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika,
Kwa ujumla Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar imefanikisha majukumu yake ya kufuatilia utekelezaji wa kazi zake katika Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara hizo ambazo zimeainishwa katika ripoti hii.

Aidha, Kamati kwa dhati kabisa inachukua nafasi hii adimu kuzipongeza Wizara na taasisi hizo, kwa juhudi zinazochukuwa katika utekelezaji wa majukumu ya kazi zao za kila siku. Sambamba na hilo, Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe katika kipindi chote kilichasalia.

Mheshimiwa Spika,
Mwisho kabisa, Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mzuri.

Mheshimiwa Spika,
Baada ya maelezo hayo machache, naomba kutoa hoja.

Ahsante,

…………………………..,
Mhe. Mohamed Ahmada Salum,
Mwenyekiti,
Kamati ya Ustawi wa Jamii,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.